Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2008 Certified

Ghorofa ya 7,Jengo la LAPF Pension Fund, Mkabala na Kijiji cha Makumbusho, Kijitonyama
S.L.P. 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255-22 2923513-18; Nukushi: +255-22 2923519
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

**TANGAZO KWA UMMA**

# WITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KISHAPU (KISHAPU WSSA) KWA MWAKA 2017/18 MPAKA 2019/20

## Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-17-001

Mnamo tarehe 3 Januari 2017 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kishapu (Kishapu WSSA) la kutaka kubadilisha bei ya huduma zake za maji kwa mwaka 2017/18 mpaka 2019/20.

Jedwali namba 1 mpaka 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

**Jedwali 1: Bei ya Sasa na inayopendekezwa kwa wateja wa dira**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa (kwa $m^3$) | Bei inayopendekezwa (kwa uniti moja ya ujazo) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 | % Ongezeko | 2019/20 |
| Majumbani | 665 | 80% | 1,200 | 3% | 1,240 | 8% | 1,340 |
| Taasisi | 900 | 69% | 1,520 | 7% | 1,632 | 16% | 1,900 |
| Biashara | 935 | 105% | 1,921 | 4% | 2,000 | 11% | 2,210 |
| Viwanda | - | - | - | - | - | - | 2,550 |
| Gati | 30 | 0% | 30 | 0% | 30 | 0% | 30 |
| Kuosha magari | | | 2,000 | 3% | 2,052 | 17% | 2,400 |

**Jedwali 2: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa ya Maunganisho mapya ya Huduma ya Maji**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei inayopendekezwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 | % Ongezeko | 2019/20 |
| Majumbani | 22,500 | 11% | 25,000 | 0% | 25,000 | 0% | 25,000 |
| Taasisi | 22,500 | 11% | 25,000 | 0% | 25,000 | 0% | 25,000 |
| Biashara | 22,500 | 11% | 25,000 | 0% | 25,000 | 0% | 25,000 |
| Viwanda | - | - | - | 0% | - | 0% | 30,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuosha magari | - | - | 25,000 | 0% | 25,000 | 0% | 25,000 |

**Jedwali 3: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kurudishiwa Huduma ya Maji**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei inayopendekezwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 | % Ongezeko | 2019/20 |
| Majumbani | 5,500 | 9% | 6,000 | 0% | 6,000 | 0% | 6,000 |
| Taasisi | 5,500 | 9% | 6,000 | 0% | 6,000 | 0% | 6,000 |
| Biashara | 5,500 | 9% | 6,000 | 0% | 6,000 | 0% | 6,000 |
| Viwanda | - | - | - | 0% | - | 0% | 6,000 |
| Kuosha magari | - | - | 6,000 | 0% | 6,000 | 0% | 6,000 |

**Jedwali 4: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa juu ya Ada ya Huduma**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei inayopendekezwa (kwa mwezi) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 | % Ongezeko | 2019/20 |
| Majumbani | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Taasisi | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Biashara | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Viwanda | - | - | - | 0% | - | 0% | 2,000 |
| Kuosha magari | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |

**Jedwali 5: Tozo ya Sasa na Inayopendekezwa ya Fomu ya Maombi Ya Maji**

| Kundi la Wateja | Bei ya Sasa | Bei inayopendekezwa (kwa fomu moja) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 | % Ongezeko | 2019/20 |
| Majumbani | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Taasisi | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Biashara | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |
| Viwanda | - | - | - | 0% | - | 0% | 2,000 |
| Kuosha magari | - | - | 2,000 | 0% | 2,000 | 0% | 2,000 |

Kutokana na wasilisho la Kishapu WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Kishapu WSSA kuweza kumudu gharama za uendeshaji kama vile malipo ya ankara ya umeme, malipo ya ankara ya maji kutoka KASHWASA (Bulk water supplier) , kuongeza mtandao wa mabomba na kukarabati mtandao wa mabomba chakavu ili kukabiliana na ongezeko la mahitaji ya maji na kuboresha huduma ya maji kwa ujumla.

Kwa mujibu wa kifungu Na.19(2)(b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na maoni ya Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Mkutano wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau utafanyika siku ya **Alhamisi** tarehe **20 Julai 2017** katika ukumbi wa **SHIRECU** mjini Kishapu kuanzia **saa 4.00 asubuhi**.

Wadau wanaopenda kutoa maoni yao kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu kabla ya tarehe **30 Julai 2017.**

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, ghorofa ya saba katika jengo la **LAPF PENSION FUND, MKABALA NA KIJIJI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA , DAR ES SALAAM** au ofisi za Kishapu WSSA zilizoko mjini Kishapu.

**Imetolewa na:**
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**
**30 Juni 2017**